

---

# EVANGELISM FOR CHRIST

## UINJILISTI KWA AJILI YA KRISTO

---

DISCIPLESHIP SERIES IV

---

FULL LIFE MINISTRY KENYA

NAME \_\_\_\_\_

**Purpose:** Provide teachings to equip the body of Christ to become warrior disciples of Jesus Christ. Since we are all living in the "Last Days" before the return of Jesus Christ, the command to "Go Make disciples...teaching them to observe all I have commanded you" is immediate.

Copyright © June 2014

Written By: Bishop Kenny Chivington – Full Life Ministry Kenya

**Madhumuni:** Kutoa mafundisho kuimarisha mwili wa kristo ili uwe mashujaa wanafunzi wa Yesu Krito. Maana tunaishi katika siku za mwisho, kabla ya kurudi kwake Yesu Krito, amri ya kwenda kuwafanya wanafunzi, kuwafundisha kushika yote tulioamriwa, ni ya dharura.

Hakimiliki © 06 2014

Mwandishi: Askofu Kenny Chivington – Full Life Ministry Kenya

These next 6 lessons have been written, that you as a follower of Jesus Christ, will be victorious in Evangelism for Christ. Each lesson is a separate study in which you will learn Truth and then with each following lesson, build a foundation of Truth that cannot be **shaken** or destroyed by this present world.

Take whatever time you need to allow the Bible's Truth to become part of you. Memorizing the Truth will build your faith and prepare you to win the battles that lay ahead of you. Memory verses are listed at the end of this book.



You now are in a battle in which hell itself desires your defeat, but Jesus Christ has already secured your victory, if you will just obey Him.

*“The thief (satan) comes to steal, kill and destroy, but I (Jesus) have come that they might have **life and life more abundantly**” John 10:10*

Masomo haya sita[6] yameandikwa, ili wewe kama mfuasi wa Yesu Kristo, uwe mshindi katika Uinjilisti kwa ajili ya Kristo. Kila somo lina utofauti ili wewe ujifunze Ukweli na pia katika kila somo, ujenge msingi wa Kweli ambao hauwezi **kutikiswa** wala kuharibiwa na ulimwengu huu wa sasa.

Chukua wakati mwafaka unaohitaji ili kuruhusu Ukweli wa Biblia kuwa sehemu yako. Kukariri huwo Ukweli utajenga imani yako na kukutayarisha[kukuandaa] kushinda vita vilivyo mbele yako. Mistari ya kukariri imewekwa mwisho wa kitabu hiki.



Sasa, uko katika vita ampapo kuzimu inatamani kushindwa kwako, lakini Yesu Kristo tayari amehifadi ushindi wako iwapo tu utatii

*“Mwizi [shetani] huja kuiba, kuuwa na kuharibu, bali Mimi [Yesu] nimekuja ili muwe na **uzima kasha nao tele**”Yohana10:10*

**Preparation - Foundation**

What you have been learning and doing is preparation Jesus requires to be His disciple. John 14:8-21 1<sup>st</sup> Do you believe that who I say I am is who I am? Then if you believe that who I say I am – I am, do you love me? {Same question Jesus asked Peter...} Then, if you love Me are you keeping my commandments? Then, if you are keeping my commandments, I (Jesus) will pray to my Father and ask Him to send the Holy Spirit to you, to dwell with you AND in you. Then, you shall receive power to be my witnesses(Acts 1:8) AND He(Holy Spirit) will teach you all things and bring to your remembrance whatsoever I have said to you. Then, as we dwell with you and in you, you will do the works that I have done AND whatsoever you ask in MY NAME that will I do. **Then “GO” and do what you have seen Me do**

Yes, I have placed my trust (my life) in Jesus Christ

Yes, I have committed all (my life) to Jesus Christ

Yes, I am living a life of obedience to Jesus Christ

Yes, I will never walk alone, my God-Holy Spirit lives in me

Yes, I will listen and obey the Master Teacher-Holy Spirit

Yes, I have power (dunimus) to do what He-Holy Spirit asks

Yes, I will do what Jesus did – make disciples *Sign Here*\_\_\_\_\_

Before we “Go” we must know what to do when we go. Let us examine the bible to see what did Jesus do and why. Luke 19:10 (to seek and to save the lost) Jesus gave Law to the proud – Grace to the humble

Mark 10:17-27 Rich young ruler: Confronted with law, offered salvation.

John 4:4-26 Woman at the well: Confronted with law, offered salvation.

John 3:1-21 Nicodemus: Confronted with the gospel, offered salvation.

The Law must pave the way for the Gospel. Romans 7:7 “I had not known sin but by the law,” Galatians 3:24 “Wherefore the law was our schoolmaster to bring us unto Christ,” Romans 3:19 “that every mouth may be stopped and all the world may become guilty before God. vs20 “Therefore by the deeds of the law there shall no flesh be justified in His sight; for by the law is the knowledge of sin.” Romans 4:15 “for where no law is, there is no transgression.” Romans 5:13”for until the law sin was in the world, but sin is not imputed when there is no law.” God said He would magnify the law in [Isaiah 42:21] and Jesus said “I am not come to destroy, but fulfill” Matthew 5:17

A person must be brought to see they are condemned before a righteous God by the law. They must acknowledge offending God by violating His holy law. Their motive for coming to Jesus must be to receive forgiveness for their sins and to flee from the wrath of God. Only by repenting, turning away from their sins and placing their trust in Jesus can this be accomplished.

Yale ambayo umekuwa ukijifunza [soma] na kufanya ni maandalizi, Yesu anakuhitaji uwe mfuasi wake. Yohana 14:8-21 Kwanza, Je! Unaamini kuwa nisemaye Mimi niliye ndiye? Ikiwa unaamini nisemaye Mimi Ndimi niliye Ndiye, Je! Wanipenda? {Swali sawa na hili Yesu alimuuliza Petro...} Ikiwa ndiyo unanipenda, unazitii amri zangu? Ikiwa unazitii amri zangu, Mimi {Yesu} nitakuombea kwa Baba yangu na kumuuliza akutumie Roho Mtakatifu, akae kwenu na ndani yenu. Nanyi mtapokea nguvu kuwa mashahidi wangu {Matendo 1:8} Na Yeye {Roho Mtakatifu} atawafundisha mambo yote na kuwakumbusha kila jambo ambalo nimewaambia. Tunapokaa kwenu na ndani mwenu, mtafanya kazi ambayo nimeifanya na lolote mtakalo uliza kwa JINA LANGU nitalifanya. **Kwa hivyo “ENENDENT” mkafanye yale ambayo mmeyaona nikiyafanya** Ndivyo, Nimeiweka imani yangu {Maisha yangu} Ndani ya Yesu Kristo Ndivyo, Nimeiweka {Maisha yangu yote} Kwa Yesu Kristo Ndivyo, Ninaiishi maisha ya utiifu kwa Yesu Kristo Ndivyo, Sitatembea pekee yangu, Mungu wangu-Roho Mtakatifu anaiishi ndani mwangu Ndivyo, Nitasikiliza na kumtii mwalimu-Roho Mtakatifu Ndivyo, Nina nguvu {dunimus} ya kufanya yale Yeye-Roho Mtakatifu anataka Ndivyo, Nitafanya kile Yesu alifanya---Kufanya wanafunzi.

*Weka sahihi hapa \_\_\_\_\_*

Kabla “Kuenenda” ni lazima tufahamu tutakalofanya tutakapoenda. Acha tutazame [Tuchambue] Biblia tuone Yesu alifanya nini na ni kwa nini. Luka 19:10 (kutafuta na kuokoa kilichopotea) Yesu aliwapa sheria wenye kiburi - Neema kwa wapole.

Marko 10:17 Kijana tajiri-kiongozi: Alikabiliana na sheria, akapewa wokovu.

Yohana 4:4-26 Mwanamke kisimani: Alikabiliana na Seria, Akapewa wokovu.

Yohana 3:1-21 Nikodemo: Alikabiliana na Injili, Akapewa wokovu.

Sheria ni lazima itengeneze njia kwa ajili ya injili. Warumi 7:7 “Walakini singalitambua dhambi ila kwa sheria,” Wagalatia 3:24 “Hivyo torati imekuwa kiongozi kutuleta kwa Kristo,” Warumi 3:19 “Ili kila kinywa kifumbwe, na ulimwengu wote uwe chini ya hukumu ya Mungu. Mstari wa 20 “Kwa sababu hakuna mwenye mwili atakayehesabiwa haki mbele zake kwa matendo ya sheria; kwa maana kutambua dhambi huja kwa njia ya sheria.” Warumi 4:15 “maana pasipokuwapo sheria hapana kosa.” Warumi 5:13 “Maana kabla ya sheria dhambi ilikuwamo ulimwenguni, lakini dhambi haihesabiki isipokuwapo sheria,” Mungu alisema ataidhihirisha sheria katika {Isaiya 42:21} na Yesu akasema “Sikuja kuitangua sheria, bali kutimiliza” Mathayo 5:1

Mtu ni lazima anogozwe aone kuwa amehukumiwa mbele ya Mungu mwenye haki kwa sheria. Ni lazima wakubali kuwa wamemkosea Mungu kwa kuihalifu sheria. Nia yao ya kuja kwa Yesu ni lazima iwe ni kupokea msamaha wa dhambi na kuhepuka ghadhabu ya Mungu. Ni kwa kutubu tu, kugeuka na kuacha dhambi zao na kuweka tumaini[imani] lao kwa Yesu ndipo hili likamilike.

## **EVANGELISM FOR CHRIST - Lesson 2** **The Approach and Preparing the Way**

8

There are unlimited ways to engage those that are without Jesus as their savior. We just need to go where they are. In the market place, in the bus, at their home, walking along the road, at the coffee shop, anywhere you can have a conversation. Let's look at how we should start.

The number 1 reason most people do not share their faith is fear. Fear of not knowing what to say, fear of rejection or fear of persecution. Let your compassion for the lost conquer your fears. The worst that may happen to you is being rejected or some sort of persecution. The worst that will happen to those that we are to "Go" to is eternal torment in the lake of fire. Let your weakness become your strength [II Corinthians 12:9-10]  
Know that God has provided "power" - not "fear" [II Timothy 1:7]

Unless someone has come to you asking spiritual direction, you will need to initiate the conversation. That is usually very easy. All of us like to be greeted with a smile and cheerful greeting. Depending on the amount of time you think you have with this person (walking down the road you will have much more time than, if you are on a bus for 10 minutes) determine your path of approach.

Let us look at how Jesus talked with someone He wanted to lead to repentance and eternal life. You will find that unless He was first asked, like with Nicodemus or the rich young ruler, he first related to the person and then created an opportunity to share the Truth.

RELATE - to whom you are speaking. [John 4:7] Comment on (the flowers; a child; the weather; what may be going on)

CREATE - an opportunity to share the gospel. [John 4:10] Have you ever wondered why God made so many different kinds of flowers? Do you know of any good churches nearby? Use a gospel tract or Commandments coin. Do you have one of these? (Determine if they are open to gospel) - Honeybee

CONVINCE - through the heart. [John 4:16] We must go around intellect to conscience (con-with; science- knowledge) Rom.2:15 God has written His law on our hearts, everyone - Right/Wrong. Unreached tribes that have not had any religious exposure know this. Psalms 19:7 says "The law of the Lord is perfect, converting the soul".

The world/satan has seared many people's consciences with man's standards (ex. compared to Idi amin Dada I'm pretty good) God's standards -The Law has not changed. (ex. Moon-Sun) We need to apply God's Law to the conscience until self-righteousness has been dismantled and the person sees themselves condemned before a Holy God. You can enable the person to see themselves as God does by the use of His law. This will make the difference of sowing seed into fertile ground or sowing seed where it will die such as onto stony ground or among the thorns[Mark 4:3-19] The law will till up the ground so that what is planted will have root and grow. Airplane-Parachute



Kuna njia nyingi za kuwafikia wale ambao hawajampokea Yesu kama Mwokozi wao. Tunahitaji tu kuenda kule waliko. Sokoni, kwenye Basi, nyumbani kwao, kutembea njiani, kwenye mkahawa[Hotelini], popote pale ambapo unaweza kuwa na mjadala nao. Acha tuone jinzi tunaweza kuanza.

Sababu ya kwanza ambayo huwafanya watu kutoshiriki imani yao na wengine ni uoga. Uoga wa kutojua jambo la kusema, Uoga kwamba watakataliwa au uoga kuwa watadhikiwa. Acha huruma wako kwa waliopotea ushinde uoga. Jambo baya ambalo laweza kutokea kwako ni kukataliwa ama namna Fulani ya dhahaka. Janga litakalo tokea kwa wale unaopaswa “kuwaendea” ni mateso ya milele katika ziwa la moto. Acha unyonge wako uwe ndiyo nguvu zako[2 Wakorintho 12:9-10] Jua ya kuwa Mungu amekupa “Nguvu[Uwezo]” Wala sio “uoga”[2Timotheo 1:7]

La sivyo mtu amekuja kwako kukuuliza mwelekeo wa kiroho, wewe unahitajika kuanzisha masungumzo. Hiyo kawaida ni rahisi. Sisi sote tunapenda kusalimiwa[kuamkuliwa] na tabasamu na salamu za furaha. Kutegemea na muda[wakati] unaodhani kuwa uko nao na mtu huyu[kutembea njiani utakuwa na wakati mwingi kuliko dakika 10 ikiwa uko kwenye Basi] Tafakari njia yako ya kuwaendea[kuanzisha masungumzo].

Hebu tutazame vipi Yesu alisungumza na mtu ambaye alitaka kumwongoza katika toba na uzima wa milele. Utagundua kuwa la sivyo kama hakuulizwa kwanza, kama Nikodemo na Yule kijana tajiri, alijifahamisha kwanza kwa mtu kasha akatengeneza nafasi ya kushiriki Ukweli.

JIFAHAMISHE - kwa mtu unayesungumza naye[Yohana 4:7] Toa mfano wa [Maua; mtoto; hali ya hewa; chochote kile ambacho kitakuwa kinaendelea kwa wakati huo].

TENGENEZA - nafasi ya kushiriki injili. [Yohana 4:10] Umewahi kujiuliza ni kwa nini Mungu aliumba aina nyingi za maua? Je! Wajua kanisa lolote nzuri karibu nawe? Tumia vijitabu vya injili au shilingi ya amri kumi. Uko na moja kati ya hizi?[Chunguza ikiwa ziko wazi kwa injili]-Nyuki ya asali.

SHAWISHI - moyoni.[Yohana 4:16] Lazima tuenende katika mzunguko wa kiakili na dhamiri[katika-Dhdmiri-ufahamu]Warumi 2:15 Mungu ameandika Torati[Amri] yake mioyoni mwetu, kila mtu—Ukweli/Uwongo. Makabila yote ambayo hayajafikiwa na kufundishwa dini yoyote wanafahamu hili. Zaburi 19:7 inasema “Sheria ya Bwana ni kamilifu, huiburudisha nafsi”

Dunuiani shetani ameteka dhamiri ya watu wengi katika viwango vya wanadamu [mfano kulinganishwa na Idi amin Dada; Mimi ni mzuri sana] Viwango vya Mungu sheria haijabadilisha[haiwezi] [mfano, Mwezi, Jua] Tunahitajika kutumia sheria ya Mungu katika dhamiri hadi haki yetu wenyewe ibomolewe na watu waone ya kuwa wamehukumiwa mbele za Mungu Mtakatifu. Unaweza kumfanya mtu ajione mwenyewe jinzi Mungu anavyomona kwa kutumia sheria ya Mungu. Hii italeti tofauti ya kupanda mbegu katika udongo wenye rutuba au kupanda mbegu pahali ambapo itakufa kama vile kwenye mwamba[mawe] au kwenye miiba[Marko 4:3-19]\_Sheria itaandaa

CONVINCE: (continued)

Let us look at paving the way by using God's law. Leading someone by the use of God's law can be challenging, but John 8:32 declares "And ye shall know the truth and the truth shall set you free". The scriptures you have memorized and placed in your heart will provide strength as you reach out to those who are lost and destined to an eternity without God. Remember, God called you to "Go" and He will enable you to do what He has asked you to do. [Acts 1:8]

This is an outline which will give you a pattern to follow. Following the Holy Spirit's leading is so very important. You are preparing yourself by having a plan of action, but the plan may need to be altered (changed) because of the condition of the heart of the person you are talking with. [1 Samuel 16:7] Only the Holy Spirit can look into the heart and determine our course (pattern) of action. Boat-Rudder

Most people you will speak with do not understand they are guilty. By using God's Law and God's Word [I John 3:4] they will be confronted with their guilt. At that point, they will have to make a decision. They will make a decision and they will either say yes to the Gospel or reject God's salvation.

-Would you consider yourself to be a good person?

-Do you think you have kept the 10 commandments?

Let's take a quick look...

-Have you ever lied? What does that make you? Lying is a violation of the 9<sup>th</sup> commandment.

-Have you ever stolen something? What does that make you? Stealing violates the 8<sup>th</sup> commandment.

-Have you ever lusted after a wo(man) Jesus said 'whosoever looketh on a wo(man) to lust after her hath committed adultery with her already in his heart.' Violates the 7<sup>th</sup> commandment. Matthew 5:28

-Have you ever hated anyone? Jesus said "Whosoever hateth his brother is a murderer" Violates 6<sup>th</sup> commandment I John 3:15

By your own admission you are a lying, thief, an adulterer and murderer at heart and we have only looked at 4 of the 10 commandments. [Hebrews 9:27]

If God judges you by the 10 commandments will you be innocent or guilty?

If God judges you by the 10 commandments will you go to heaven or hell?

Good Judge-Murderer

Does that concern you? If, Yes. We discern if yes as truth, and then we can present the Gospel. If, No. (No mean no or means I am struggling) You will need to discern and either part on a positive note such as "Thanks, John, for being honest and John...please give some more consideration to what we discussed" or "You know John, I really believe deep down in your heart you really are concerned. John, God loves you." Then proceed with the Gospel, but remember you are there to present, not demand.

**Kutengeneza njia kwa Injili**

KUSHAWISHI: [Inaendelea]

Acha tutazame kutengeneza njia kwa kutumia sheria ya Mungu.

Kumuelekeza mtu kwa kutumia sheria ya Mungu inaweza kuwa na changamoto, lakini Yohana 8:32 inasema “Tena mtaifahamu kweli, nayo hiyo kweli itawaweka huru”. Mistari ambayo umekariri na kuweka moyoni mwako itakupa nguvu wakati utawaenda waliopotea na wanaelekea katika milele bila Mungu. Kumbuka Mungu alikuwa “uenende” na atakuwezesha kufanya yale anayokuuliza kuyafanya.[Matendo 1:8]

Huu ni mwelekeo ambao utakupatia njia ya kufuata. Kufuata mwongozo wa Roho Mtakatifu ni muhimu sana. Unajiandaa mwenyewe kwa kuwa na mpango wa kutenda, lakini mpangilio huo unaweza kuwa na marekebisho[mabadiliko] kwa sababu ya hali ya moyo wa mtu unayesungumza naye. [1 Samweli 16:7] Roho Mtakatifu pekee anaweza kuangali moyo na kuelewa namna[njia] yetu ya kutenda. Mashua-Makasia

Watu wengi ambao utaoengea nao hawaelewi kuwa wana hatia. Kwa kutumia sheria ya Mungu na neno Lake[1 Yohana 3:4] watakabiliana na hatia yao. Katika hali hiyo watahitajika kufanya uamuzi. Watafanya uamuzi na pengine kusema ndiyo kwa injili au kukataa wokovu wa Mungu.

-Je! Wajiona mwenyewe kuwa mtu mzuri?

-Je! Wafikiri umeziweka[Umezingatia] amri kumi?

Acha tutazame kwa haraka.....

-Umewahi kudanganya? Hiyo inakufanya wewe kuwa nani? Kudanganya ni kuhalifu amri ya Tisa[9] ya Mungu.

-Umewahi kuiba kitu? Hii inakufanya wewe kuwa nani? Kuiba ni kuvunja amri ya Nane[8] ya Mungu.

-Umewahi kumwangukia mwanamke kwa kumtamani? Yesu alisema “Kila mtu atazamaye mwanamke kwa kumtamani, amekwisha kuzini naye moyoni mwake” Hiyo ni kuvunja amri ya saba[7] Mathayo 5:28

-Umewahi kumchukia mtu yeyote? Yesu alisema, “Kila amchukiye ndugu yake ni muuaji” Anavunja amri ya Sita[6] ya Mungu 1 Yohana 3:15

Kwa kukubali kwako[kukiri] wewe ni mwongo, mwizi, mwasherati na muuaji moyoni na tumetazama nne[4] tu kati ya amri kumi[10]. [Waebrania 9:27]

Iwapo Mungu atakuhukumu kwa amri kumi[10], je! Utakuwa na hatia au la?

Iwapo Mungu atakuhukumu kwa amri kumi[10], je! Utaenda mbinguni au jehnamu?

**Mwamuzi mzuri-Muuaji**

Hiyo inakuhusu wewe? Ikiwa, Ndiyo. Tunatambua ndiyo kuwa ni kweli, na sasa tunaweza kuileta injili. Ikiwa, La. [La inamaanisha la au ninajaribu] Utahitajika kutambua na pengine kwa mfano kusema “ Ahsante, Yohana, kwa kuwa mwaminifu na Yohana...tafadhali tilia maanani yale ambayo tumesungumza” au “ Unajua Yohana, Ninaamini moyoni mwako hakika kuwa unatafakari[Unafikiria kuhusu hayo]. Yohana, Mungu anakupenda.” Kisha endelea na injili, lakini kumbuka uko hapo kuleta injili wala sio kwa kulazima.

**REVEAL** – Share the Good News of Jesus Christ [John:4:26] When a sinner sees himself condemned and under eternal judgment, it is then that he will come to the cross where he will meet the One who paid his debt. There are many ways to share and/or illustrate the gospel, but always remember there is only one true gospel.

Everyone has sinned [Romans 3:23; Isaiah 53:6] We are all in the same boat and it is sinking [Roman6:23a; Hebrews 9:27] God loves you and has provided payment for all of your of sins [Romans 6:23b; Romans 5:8] Jesus paid in full your debt on the cross [John 3:16; I Peter 3:18] You must place your trust (faith) in Jesus and what He did for you [Ephesians 2:8-9; Titus 3:5] You will need to repent of your past life of sin [Luke 13:3; Mark 6:12] Repentance is not just to stop sinning, but changing your mind about sin. You will want to start to love the things God loves and hate the things God hates. (Illustrate – Repentance)

Do you want to accept what Jesus has done for you and receive Jesus Christ into your life? What you are about to do will be the most important decision in your entire life. It will determine where you will spend eternity. Romans 10:9 says “That if thou shalt confess with thy mouth the Lord Jesus Christ and shalt believe in thine heart that God hath raised him up from the dead, thou shall be saved.” Confession is confessing the truth about whom you have been and who you are right now. Admitting to God that you are a sinner and that you need a savior. Placing your trust in what Jesus has done for you on the cross and turning away from all sin.

After giving instruction, encourage the person to pray what is in their heart. Again you will need to discern what is going on. If they are hesitant to pray, it may be that they have never prayed and do not know how to pray. You may need to ask a discerning question. Or they may be wrestling with the grip of sin on their life at that very moment. If so, pray for them and pray as the Holy Spirit leads you. This is where you find that the time you have spent in prayer before going out to share Jesus, is so very critical. At this point, the person may calmly and joyfully confess, repent and accept Jesus as their savior. Or you may encounter demonic oppression. No matter what the circumstance though, you are not alone because the Holy Spirit will guide you. Again, the necessity of a lifestyle of prayer will reveal itself as God uses you to do what He asks.

When you see that the person has truly called on God and they have finished praying (The workings of God are not on a time watch) you will want to encourage them and do some cultivating. Share with them two or three scriptures such as [I John 5:13; John 5:24; Romans 8:1] If they do not have a bible, if possible, give them one. Welcome them into the family of God. Invite them to church. Share with them that you're church has free teachings to help them in their new life and that you are willing to help them learn. Let them know not only does God love them, but you love them.

**Kutangaza wazi injili**

WEKA WAZI - Shiriki habari njema ya Yesu Kristo[Yohana 4:26] Wakati mwenye dhambi anajiona mwenyewe kuwa amehukumiwa na ako chini ya hukumu ya milele, hapo ndipo atakapo kuja msalabani na kukutana na Yule[Yesu] aliyemlipia deni. Kuna njia nyingi za kushiriki na kueleza injili, lakini kila mara ukumbuke kuwa kuna injili moja tu ya kweli.

Sisi sote tumetenda dhambi[Warumi 3:23; Isaiya 53:6] sisi sote tuko katika mashua moja ambayo inazama[Warumi 6:23a; Waebrania 9:27] Mungu anakupenda na amelipa gharama[Deni] kwa ajili ya dhambi zako zote[Warumi 6:23b; Warumi 5:8] Yesu amelipa kikamilifu deni lako msalabani[Yohana 3:16; 1 Petro 3:18] Ni lazima uweke tumaini [imani] yako kwa Yesu na kile alichokufanyia[Waefeso 2:8-9; Tito 3:5] Utahitajika kutubu maisha yako ya kale ya dhambi[Luka 13:3; Marko 6:12] Kutubu sio kuacha tu dhambi bali ni kubadilisha mawazo[Nia] yako kuhusu dhambi. Utahitajika kuanza kupenda vitu ambavyo Mungu anapenda na kuchukua vitu ambavyo Mungu anavichukia. (onyesha – toba)





Je! Ungependa kukubali kile Yesu amekutendea na kumpokea Yesu Kristo maishani mwako? Kile ambacho unataka kukifanya ni uamuzi muhimu sana katika maisha yako yote. Itaonyesha kule utakaa milele. Warumi 10:9 inasema “Kwa sababu ukimkiri Yesu kwa kinywa chako ya kuwa ni Bwana, na kuamini moyoni mwako ya kuwa Mungu alimfufua katika wafu, utaokoka.” Kukiri ni kusema ukweli kuhusu kule ulikokuwa na hapa uliko sasa. Kuungama[kukubali] mbele za Mungu kuwa wewe ni mwenye dhambi na kuwa unahitaji Mwokozi. Kuweka tumaini[imani] yako kwa kile Yesu amekutendea msalabani na kugeuka na kuacha dhambi zote.

Baada ya kupeana mwongozo, mtie moyo mtu aombe yalioko moyoni mwake[mwao]. Tena utahitajika kutambua kinachoendelea. Iwapo wanasitasita kuomba, pengine hawajawahi kuomba au hawajui jinzi ya kuomba. Utahitajika kuwauliza swali ili utambue[ujue] hilo. Ama labda watakuwa wanamenyana na msukumo wa dhambi maishani mwao wakati huo. Ikiwa ni hivyo, waombe jinzi Roho Mtakatifu atakavyo kuongoza. Hapo ndipo utagundua ya kuwa muda ambao umeutumia katika maombi kabla ya kwenda nje kushiriki Yesu ni muhimu sana. Wakati huu, mtu anaweza kwa upole na furaha kukiri, kutubu na kumkubali Yesu kama Mwokozi wake[wao]. Ama unaweza kukutana na kupagawa na mapeto. Haijalishi ni hali gani utakumbana nayo, hauko pekee yako kwa sanabu Roho Mtakatifu Atakuongoza. Tena maisha ya uombezi yatajidhihirisha yenyewe Mungu anapokutumia kufanya kile Anachokuuliza.

Utakapoona mtu amemwita Mungu kwa kweli na amemaliza kuomba [Kufanya kazi kwa Mungu hukuna kipimo cha wakati] utahitaji kuwatia moyo na yowakuza. Shiriki nao vifungu viwili au vitatu vya Biblia kama vile [1 Yohana 5:13; Yohana 5:24; Warumi 8:1] Iwapo hawana Biblia, wape moja ikiwezekana. Wakaribishe katika jamii ya Mungu. Wakaribishe kanisani. Shiriki nao na uwaambie kuwa kanisa lenu lina mafundisho ya bure ya kuwasaidia katika maisha yao mapya na kuwa uko tayari kuwasaidia kujifunza[kuelimika]. Acha wajue kuwa sio Mungu pekee anayewapenda, bali wewe pia unawapenda.

**EVANGELISM IN CHRIST - Lesson 5**  
**Gospel Illustration**

There are times when using an illustration is a better way of showing the gospel.



Wakati mwingine kutumia maelezo [michoro] ni njia nzuri ya kufundisha injili.



**Mtu Mwenye**

<b>Dhambi</b>
<b>Dhambi</b>
Warumi 3:23

**MUNGU**

<b>Mtakatifu</b>
------------------

Mtu mtenda dhambi-Mungu  
 Mtakatifu  
 Kutengwa ni sababu ya dhambi  
 Waefeso 2:8-9



**Mtu Mwenye**

<b>Dhambi</b>
<b>Dhambi</b>
Warumi 3:23
<b>Mauti</b>
Warumi 6:23
<b>Hukumu</b>
Waebrania 9:27

**MUNGU**

<b>Mtakatifu</b>
------------------

Mtu mtenda dhambi-Mungu  
 Mtakatifu  
 Kutengwa ni sababu ya dhambi  
 Mtu hujaribu kumfikia Mungu kwa matendo  
 Matendo yote hupungukiwa  
 Mshahara wa dhambi ni mauti  
 Sote tutakufa-Kisha hukumu  
 Mauti milele



**Mtu Mwenye**

**YESU**

**MUNGU**

<b>Dhambi</b>
<b>Dhambi</b>
Warumi 3:23
<b>Mauti</b>
Warumi 6:23
<b>Hukumu</b>
Waebrania 9:27

<b>Mtakatifu</b>
<b>Upendo</b>
Warumi 5:8
<b>Yesu</b>
I Petro 3:18

Mungu anadhihirisha upendo Wake kwetu  
 Mungu anapeana Njia  
 Yesu alikufa kwa ajili yetu  
 Yesu alitulipia gharama[deni]



**Mtu Mwenye**

**YESU**

**MUNGU**



<b>Dhambi</b>
<b>Dhambi</b>
Warumi 3:23
<b>Mauti</b>
Warumi 6:23
<b>Hukumu</b>
Waebrania 9:27

<b>Mtakatifu</b>
<b>Upendo</b>
Warumi 5:8
<b>Yesu</b>
I Petro 3:18
<b>Uzima wa Milele</b>
Yohana 5:24

Mungu anadhihirisha upendo Wake kwetu  
 Mungu anapeana Njia  
 Yesu alikufa kwa ajili yetu  
 Yesu alitulipia gharama[deni]  
 Hatutahukumiwa kwa ajili ya dhambi zetu  
 Sasa una uzima wa milele

**Objections – How to handle them**

The first preparation to handle objections is prayer. Pray that God will open the hearts of those who you will be talking to. Pray for His love to be seen in you and that He would give you His wisdom for whatever situation you may find yourself. [I John 3:18; Proverbs 3:5-6]

Why do they bring objections? Let's see what the bible says. I Corinthians 2:14 "the natural man receiveth not the things of the Spirit of God; for they are foolishness unto him; neither can he know them, because they are spiritually discerned" John 3:19 "Men love darkness rather than light, because their deeds are evil" Some are more interested in the honor of men than God [John 5:44] Many are deceived and follow a way that seems right [Proverbs 14:12] Some have rejected God often and have even been spiritually blinded [John 12:37-40]

We should expect that we will meet with objections. For this reason, we are commanded to be ready [I Peter 3:15] This defense is possible because, unlike other religions, the Bible has the advantage of absolute truth in every respect.

Next, establish these rules for yourself. Never argue. Instead, negotiate the objection.

Example 1. I do not believe there is a heaven. = I can understand how you might feel that way, but I think we could agree there are some other important matters involved. So, if there were a heaven, when you die, you would want to go there, right? Do not show anger or irritability. Show love and patience. If question will be answered later in presentation, tell them you be coming to that soon...return to where you were.

Example 2. I do not believe the Bible. = You don't believe the bible? Well that certainly is your privilege, but if the bible is true you must accept the consequences. So, if the bible were true, you would want to know what God is speaking to you, right? Another answer: From your objection, I must conclude that you have not studied its pages. The Bible is perfect its accuracy of history, its perfect accuracy of its prophecies, not one scientific or medical inerrancy, with no contradiction or evidence found in geology, paleontology or archaeology, you must conclude that it is reliable by definition.

Example 3. Maybe later – Not now = You do have the right to reject God's offer by putting off your decision to accept it, but with that you alone will bear the consequences of your decision. None of us are assured even our next breath. The bible says "now is the accepted time; behold, now is the day of salvation" [II Corinthians 6:2]

Example 4. I do not believe in hell = Jesus spoke more about hell than any other author in the entire bible. Why? He had 1<sup>st</sup> hand knowledge. He created it. So on this one; you don't want to be wrong. If there is a hell, would you agree that you would not want to go there?

Example 5. There are many ways to heaven = No one; nowhere; ever provided the only sacrifice acceptable to God for admission to heaven. Only the perfect, sinless Son of God-Jesus could be that sacrifice. [John 14:6]



**Pingamizi – Jinzi ya kukabiliana nazo**

Maandalizi ya kwanza ya kukabiliana na pingamizi ni maombi. Omba ya kwamba Mungu atafungua mioyo ya wale utakaosungumza nao. Omba ili kwamba upendo Wake uonekane ndani mwako na kuwa atakupa hekima Yake kwa hali yoyote ile utakayo patikana ndani. [1 Yohana 3:18; Mithali 3:5-6]

Kwa nini waleta pingamizi? Hebu tuone kile Biblia inasema. 1 Wakorintho 2:14 “Basi mwanadamu wa tabia ya asili hayapokei mambo ya Roho wa Mungu; maana kwake ni upuzi, wala hawezi kuyafahamu, kwa kuwa yatambulikana kwa jinzi ya rohani” Yohana 3:19 “ Na watu wanapenda giza kuliko nuru; kwa maana matendo yao yalikuwa maovu” Wengine wanajali kuheshimiwa na watu kuliko Mungu [Yohana 5:44] Wengi wamedanganywa na kufuata njia anayoonekana kuwa ni sawa machoni pao [Mithali 14:12] Wengine wamemkataa Mungu na sasa wamepofuka kiroho [Yohana 12:37-40]

Lazima tutarajie kuwa tutakutana na pingamizi. Kwa sababu hii, tunaamriwa tuwe tayari [1 Petro 3:15] Kinga hii inawezekana, kinyume na dini [Kanuni] zingine, Biblia ina zaidi ya ukweli wa kila jambo. Pili, anzisha mwongozo [sheria] hizi mwenyewe. Usiwe mbishi. Badala yake, jadili hiyo pingamizi.

Mfano 1. Siamini kama kuna mbingu. = Ninaweza kuelewa ni kwa nini unahisi hivyo, lakini ninafikiri tutakubaliana kuwa kuna mambo mengine muhimu ambayo yanahusika. Kwa hivyo kama kungalikuwa na mbingu, wakati utakufa, ungelipenda kuenda huko, kweli? Usionyeshe hasira au taharuki. Unyesha upendo na uvumilivu. Ikiwa maswali yatajibiwa baadaye katika mjadala, waambie kuwa utarejelea hapo hivi karibini.....rudi pale ulipokuwa.

Mfano 2. Siamini Biblia = Hauamini Biblia? Hiyo kweli ni haki yako, lakini ikiwa Biblia ni kweli basi ni lazima ukubali matokeo yake. Kwa hivyo, iwapo Biblia ingelikuwa kweli, ungelitaka kujua kile Mungu anachokuambia, sivyo? Jibu jingine: Kutokana na pingamizi yako, ninaamini ya kuwa bado haujasoma kurasa zake. Biblia haina kasoro, ni hakika ya historia, ni kweli na hakika ya unabii wake, hakuna shaka ya sayanzi, sayanzi ya kimatibabu, haina kuchanganyikiwa au ushahidi kutokana na Jiolojia [sayanzi yam awe na mchanga], utafiti wa mabaki ya wanyama na mimea ama, utafiti wa tamaduni za kale, lazima uamini kuwa ni ya kutegemewa kwa ufafanuzi.

Mfano 3. Pengine baadaye - Sio sasa = Una haki ya kumkataa dhawabu ya Mungu kwa kuweka mbali uamuzi wa kuikubali, lakini kwa hiyo wewe pekee yako utabeba hasara ya huo uamuzi. Hakuna hata mmoja wetu ana hakika hata ya punzi atakayopumua baadaye. Biblia inasema “ Wakati uliokubalika ndio sasa; tazama siku ya wokovu ndio sasa” [2 Wakorintho 6:2]

Mfano 4. Siamini Jehanamu = Yesu alisungumzia sana kuhusu Jehanamu kuliko mwandishi yoyote Yule katika Biblia yote. Kwa nini? Alikuwa na habari kamili. Aliiumba. Kwa ajili ya hii; hutakikani kutenda dhambi. Ikiwa kunayo Jehanamu, je! Utakubali kuwa hutataka kwenda huko?

Mfano 5. Kuna njia nyingi za kwenda mbinguni = hakuna hata mmoja; Hakuna popote; Kuwahi kupeana dhabihu ya pekee iliyokubalika na Mungu ili kuingia mbinguni. Mkamilifu pekee, asiye na dhambi, mwana wa Mungu-Yesu ndiye hiyo dhabihu. [Yohana 14:6]

## LESSON ASSIGNMENTS

18

### Lesson 1 – Ten Commandments

- |  |                                     |
|--|-------------------------------------|
| 1.Thou shalt have no other gods before me    | 6.Thou shalt not murder             |
| 2.Thou shalt not make any graven images      | 7.Thou shalt not commit adultery    |
| 3.Thou shalt not use the Lord’s name in vain | 8.Thou shalt not steal              |
| 4.Thou shalt keep the Sabbath holy           | 9.Thou shalt not bear false witness |
| 5.Honor thy father and thy mother            | 10.Thou shalt not covet             |

Enlist two Christians to pray for you (For this class & when you “Go”)  
Commit to praying for those you will speak with

### Lesson 2 – Hebrews 9:27

Question: 1. How do you start a conversation with someone to share the gospel?

Question: 2. Why do we want to address the heart instead of the conscience?

Somo la Kwanza - AMRI KUMI

- |  |                                   |
|--|-----------------------------------|
| 1. Usiwe na miungu mingine ila Mimi        | 6. Usiue                          |
| 2. Usijifanyie sanamu ya kujonga           | 7. Usizini                        |
| 3. Usilitaje bure jina la Bwana Mungu wako | 8. Usiibe                         |
| 4. Ikumbuke siku ya sabato uitakase        | 9. Usimshuhudie jirani yako uongo |
| 5. Waheshimu baba yako na mama yako        | 10. Usitamani                     |

Weka wakristo[washiriki] wawili wakuombee[kwa ajili ya darasa hili na kisha “Uenendu”]

Waombee wale utakao enda kusungumza nao

Somo la Pili -Waebrania 9:27

Swali: 1. Je! Utaanza vipi masungumzo na mtu ili kushiriki injili naye?

Swali: 2. Ni kwa nini tunahitaji kusungunza[kuponya] moyo badala ya dhamiri?

## LESSON ASSIGNMENTS

20

Lesson 3 – Romans 5:8

Question: 1. How do we bring a person to understand they are guilty before God?

Question: 2. Did Jesus do away with the law? Give example.

Lesson 4 – I Peter 3:18

Question: 1. Explain what repentance means:

Question: 2. What are the 3 things a person must do to be saved?

Somo la Tatu - Warumi 5:8

Swali: 1. Vipi tutamfanya mtu aelewe hatia aliyonayo mbele za Mungu?

Swali: 2. Je! Yesu aliitanzua[futilia mbali] sheria[torati]? Toa mfano.

Somo la Nne - 1Petro 3:18

Swali: 1. Eleza maana ya kutubu

Swali: 2. Ni mambo yapi matatu ambayo mtu anapaswa kuyafanya ili aokolewe?

## LESSON ASSIGNMENTS

Lesson 5 – John 5:24

Question: 1. What are 3 things you need to explain about man?

Question: 2. How does man cross the bridge to God?

Lesson 6 – Ephesians 2:8-9

Question: 1. What is the most important thing to do to prepare for objections?  
Also explain, why.

Question: 2. What are two things you should never do when handling objections?

Somo la Tano - Yohana 5:24

Swali: 1. Ni mambo yapi matatu[3] unahitajika kuelezea kuhusu mtu?

Swali: 2. Ni jinzi gani mtu anavuka daraja ili amfikie Mungu?

Somo la Sita - Waefeso 2:8-9

Swali: 1. Ni jambo gani muhimu unalopswa kufanya unapojiandaa kwa ajili ya pingamizi? Pia eleza ni kwa nini.

Swali: 2. Ni mambo yapi mawili ambayo hupaswi kuyafanya wakati wa kukabiliiana na pingamizi?

These lessons can be copied and distributed *free of charge* in their original format for the making and building up of disciples of Jesus Christ.

Jesus Christ has already paid in full... your sin debt.

Masomo haya yanaweza kunakiliwa na kusambazwa bure bila malipo kati hali yake ya awali kwa ajili ya kuwafanya na kuwajenga wanafunzi wa Yesu Kristo.

Kristo Yesu tayari amelipa deni ya dhambi zenu